# Maofisa mifugo Singida wapewa msaada pikipiki

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi imeikabidhi Halmashauri ya Manispaa ya Singida pikipiki tatu kwa ajili ya maofisa mifugo ngazi ya kata, lengo kuu likiwa ni kuboresha utoaji wa huduma za mifugo katika kata zilizopo pembezoni.

Mstahiki Meya wa Manispaa ya Singida, Yagi Kiaratu, akipokea pikipiki hizo aliwataka maofisa mifugo waliokabidhiwa kuzitumia kwa malengo yaliyokusudiwa na siyo vinginevyo.

"Ninaamini huduma za mifugo katika kata zenu na kata jirani zitaimarika na wananchi watanufaika kwa elimu ya ufugaji bora pia huduma za dawa za mifugo," alisema.

Pikipiki hizo zimepelekwa katika Kata ya Uhamaka, Mtipa na Mtamaa ambapo pia maofisa hao watatoa huduma kwenye kata jirani baada ya kuwezeshwa vyombo hivyo vya usafiri.

Kiaratu aliwataka maofisa ugani kushirikiana katika kuhakikisha huduma za ugani zote zinaimarika ikiwa ni pamoja na kusimamia ukusanyaji wa mapato yatokanayo na mifugo na kilimo katika kata zao.

Awali, Mkurugenzi wa Manispaa ya Singida Jeshi Lupembe, alifanya kikao na watumishi ngazi ya kata akihimiza masuala mbalimbali ikiwa ni pamoja na usimamizi shirikishi wa miradi, kubaini vipaumbele vya kata, masuala ya usafi na mazingira, ukusanyaji mapato na kuwakumbusha wajibu wa kila mmoja katika eneo lake la kazi.

"Shirikianeni wote katika kusimamia miradi ya maendeleo, kuainisha vipaumbele vya kata, pia suala la usafi na mazingira na ukusanyaji wa mapato sitakuwa tayari kuwajibishwa kwa ajili ya uzembe wa watu wachache mimi najituma na nyinyi mjitume," alisisitiza.

Hivyo, aliwataka watumishi kuhimiza wananchi kusafisha maeneo kuzunguka nyumba zao na mitaro pamoja na barabara mbele ya nyumba zao ili kuepuka magonjwa ya mlipuko katika kipindi hiki cha mvua.

CamScanner

# Serikali yatoa bil 65/- ufugaji samaki, uvuvi

**Na Nashon Kennedy, Mwanza**

SERIKALI imetoa Sh bilioni 65 zilizotumika kuwawezesha wavuvi nchini kukopeshwa boti 158 zenye vifaa vya uvuvi sanjari na kufanya ufugaji wa vizimba, ambapo vizimba 615 vimeanzishwa kwa ajili ya ufugaji wa samaki.

Hayo yalisemwa juzi jijini Mwanza na Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Amos Makalla alipokuwa akitunguа mkutano maalumu wa wadau wa sekta ya uvuvi.

Alisema kati ya fedha hizo zilizotolewa na serikali kwa ajili ya kuwezesha shughuli za ufugaji wa samaki na uvuvi, Mkoa wa Mwanza ulipata boti 29 ukiwamo mradi wa ufugaji samaki kwa vizimba 375.

Katika hatua nyingine, Makalla alitangaza vita dhidi ya watu wanaojihusisha na vitendo vya uvuvi haramu ambapo alitoa muda wa siku saba kwa wavuvi wote wenye zana haramu za uvuvi kuziwasilisha mara moja.

Alisema watakaokaidi kuwasilisha zana haramu za uvuvi msako mkali dhidi yao utaanzishwa kwa kuwasaka watu wanaojihusisha na vitendo hivyo ili hatua kali za kisheria zichukuliwe dhidi yao.

Sanjari na agizo hilo, aliwataka viongozi wa ngazi zote katika Mkoa wa Mwanza kwa halmashauri kuhakikisha kuwa wanatimiza wajibu wao kwa kutoa elimu ya uvuvi haramu ikiwemo kulinda mazalia ya samaki na rasilimali ya ziwa Victoria dhidi ya uchafuzi wa mazingira.

Alilitaka jeshi la polisi mkoani Mwanza na malaka zingine za serikali kuhakikisha kuwa zinadhibiti zana za uvuvi zisizokubalika ili zisitumiwe na wavuvi kuvua na kufafanua kuwa uwepo wa bidhaa humo.

"Elimu itolewe mara kwa mara ili jamii ifahamu madhara ya uvuvi haramu unaofanywa katika ziwa Victoria linalotegemewa kwa ajili ya ukuzaji uchumi," alisema.

Kwa upande wake, Mtafiti Mwandamizi kutoka Taasisi ya utafiti wa Uvuvi nchini (Tafiri), Hillary Mrosso alisema kuwa utafiti kwa njia ya teknolojia ya wingi unaonesha kuwa wingi wa samaki aina ya Sangara katika Ziwa Victoria umepungua kutoka tani 621, 254 mwaka 2015 hadi tani 161, 918 mwaka 2022 huku miaka ya 2018, 2021 na 2022 ikiongozwa kwa upungufu wa aina hiyo ya samaki.

"Wingi wa dagaa umeonekana kupungua kutoka tani 859, 931 mwaka 2015 hadi 321, 392 mwaka 2017 na kwamba wingi wa uduvi umekua ukiongezeka katika vipindi mbalimbali," alifafanua Mrosso.


THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MINISTRY OF INDUSTRY AND TRADE

FAIR COMPETITION COMMISSION

NOTIFICATION REGARDING THE INTENTION OF WANANCHI CABLE (T) LIMITED TO ACQUIRE ASSETS OF WANANCHI GROUP TANZANIA LIMITED

# Uchumi wa Buluu wajieleza walivyotumia fedha za Covid 19

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) imesema Wizara ya Uvuvi na Uchumi wa Buluu imetumia vizuri fedha za Covid 19 kwa kuwawesha wananchi kuingia katika uvuvi wa mazao ya baharini.

Fedha hizo kiasi cha Sh bil 36 zimetumika pia katika ujenzi wa mabwawa 100 ya kufuga samaki na matango bahari.

Waziri wa wizara hiyo, Suleiman Masoud Makame alisema hayo wakati akitoa taarifa ya miaka mitatu ya uongozi wa Rais Dk Hussein Mwinyi na mafanikio yake.

Alisema uvuvi wa buluu na mazao ya baharini ni sehemu ya maono ya Rais wa Zanzibar Dk Mwinyi ya kuona wananchi wananufaika na rasilimali za baharini.

Alifahamisha katika kipindi cha miaka mitatu jumla ya mabwawa 100 yamejengwa kwa ajili ya ufugaji wa mazao ya baharini ikiwemo matango Bahari, samaki na kaa.

Makame alisema Sh bilioni 1.7 zimetumika kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa hayo ikiwa ni sehemu ya mikakati ya kuwawezesha wananchi ikiwemo wajasiriamali katika ufugaji wa mazao ya baharini na kuzalisha ajira za moja kwa moja 1,800.

Aidha alitoa habari njema kwa wazalishaji wa dagaa ambapo kiwanda cha kuchakata na kusarifu dagaa kimekamilika kwa asilimia 60 tayari kuanza uzalishaji wake.

Kwa mfano alisema hivi sasa soko la samaki aina ya dagaa lipo kubwa katika nchi mbali mbali ikiwemo Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo kwa hiyo kuwepo kwake ni msaada mkubwa kwa wajasiriamali.

Mapema Makame aliwaambia waandishi wa habari kwamba Wizara ipo katika mikakati ya kulinda maeneo ya hifadhi ya bahari kwa ajili ya kuona viumbe vya baharini ikiwemo matumbawe maisha yake yanakuwa ya uhakika.

Alisema kuwepo kwa hifadhi hizo kwa kiasi kikubwa zitasaidia kudhibiti na kupambana na uvuvi haramu katika maeneo hayo na hivyo kutishia maendeleo ya uchumi wa buluu na tija kwa wananchi.

CamScanner